# COUNTY GOVERNMENT OF WEST POKOT

# HOTUBA YA MHESHIMIWA SIMON KACHAPIN KITALEI, C.B.S., E.G.H., GAVANA, KAUNTI YA POKOT MAGHARIBI,

## KATIKA MAADHIMISHO YA MASHUJAA,

## TAREHE 20/10/2024

**Mabibi na Mabwana,**

Nina furaha kujumuika nanyi leo, tunapoadhimisha siku ya Mashujaa ya sitini na moja tangu nchi yetu ya Kenya ilipofikia utawala wa kibinafsi. Hii ni siku maalum ambayo tunawakumbuka na kuwaenzi mashujaa wote waliojitolea kwa ajili ya taifa letu kuu.

Ni siku muhimu ya kuukumbuka ushujaa wa kujitolea na kujinyima kwa wanawake, vijana na wanaume wa taifa hili walioliipigania na kulikomboa kutoka kwenye minyororo ya ukoloni. Tunatambua kila mmoja aliyechangia kwa njia moja au nyingine katika mabadiliko makubwa kwenye nyanja za uongozi, siasa, jamii, biashara, uchumi na maendeleo kwa ujumla. ***Asanteni sana!***

**Wananchi Wenzangu,**

Kauli mbiu ya mwaka huu, ***"Makao Nafuu kwa Wananchi Wetu,"*** inaonyesha juhudi zetu za kuhakikisha kwamba kila mkenya anapata makaazi salama na yenye heshima. Hii ni dhamira ya serikali hii kuimarisha maisha ya wananchi kwa kuwapatia mazingira bora ya kuishi katika nchi yetu, si tu mazingira bora bali pia ustawi wa jamii.

Kama vile wazee wetu walivyojitolea kupigania uhuru na mafanikio ya taifa hili, ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa hakuna hata mmoja wetu anayewachwa nyuma katika jitihada za kuleta maendeleo na usawa katika jamii.

Kwa hivyo, kuwepo kwa makao nafuu unalenga kupunguza pengo kati ya wakenya wa mapato ya juu na ya chini, pamoja na kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa makaazi. Hatua hii inalenga kulinda haki za kiuchumi za Wakenya, na kuwawezesha kuishi katika mazingira salama bila kuhatarisha amani yao.

**Mabibi na Mabwana,**
Serikali yangu inajitahidi kushughulikia changamoto ya makaazi na kuchochea umiliki wa nyumba nafuu kwa wakaazi wa kaunti yetu. Hadi sasa, tumetambua maeneo mbalimbali katika kaunti yetu, ambayo yatafanikisha mradi huu.

Aidha, nimebuni kamati maalum itakayohusika na utekelezaji wa mradi huu. Tayari jopo limeidhinishwa na kamati ya ujenzi ya bunge la kaunti, na kwa sasa linasubiri kuchapishwa katika gazeti rasmi la serikali. Majukumu ya kamati hii ni pamoja na kuratibu, kupanga, na kutekeleza mipango ya ujenzi wa nyumba nafuu ili kuhakikisha kwamba, mradi huu unaendana na malengo ya kiuchumi na matarajio ya wakaazi wa kaunti yetu.

Katika juhudi zetu za kuchangia uwepo wa nyumba nafuu katika kaunti yetu, tayari tumeweka kando shilingi milioni 50 katika mwaka huu wa kifedha kwa ajili ya kununua mabati. Mabati haya yatasambazwa katika wadi zote, yakilenga kuwasaidia jamii zetu kwa kuboresha viwango vyao na kuwapeleka kwenye nyumba za kisasa.

Mpango huu unalenga kuboresha maisha ya watu wenye mahitaji maalum kwa kuwapata mazingira safi na makazi bora, ambayo ni haki ya kila mtu. Kwa kushughulikia hitaji hili, tunakuza usalama na hali nzuri ya makaazi kwa wote, na hivyo tunachangia katika kujenga jamii yenye usawa zaidi.

**Wazalendo Wenzangu,**
Tunaposherehekea siku hii ya leo, ni nafasi nzuri ya kutafakari mafanikio tuliyoyapata na juhudi tulizoweka tangu kuasisiwa kwa mfumo wa ugatuzi. Safari yetu kama Kaunti ya Pokot Magharibi imejaa mabadiliko na maendeleo.

Tumewekeza kwa kiwango kikubwa katika miundombinu, sekta ya afya, elimu, kilimo, na masuala mengine muhimu yanayogusa maisha ya wakaazi wa kaunti hii.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa hatungeafikia mafanikio haya yote bila kuwepo amani na ushirikiano na watu wenye nia njema. Tumeshirikiana na wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na majirani zetu kuafikia amani ndani na nje ya kaunti yetu.

Japo tumeafikia mengi ya kujivunia siku hii, lazima kwa pamoja tujitokeze na kulaani maovu yanayoweza kuturudisha nyuma na kutatiza umoja wetu. Tukizingatia hayo, tunashtumu vikali tukio la hivi karibuni eneo la Amolem, wadi ya Masol la kulipuliwa na kuuliwa kwa mifugo.

Matukio kama haya hayana nafasi katika kaunti yetu, na ni lazima tujitahidi kufikia mustakabali bora ili tusishuhudie tena maovu kama haya katika jamii yetu.

Tunasihi mashirika husika kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya waliohusika na ukatili huu. Kwa pamoja, tuendelee kushirikiana katika kutafuta amani na maendeleo kaunti yetu.

## Wananchi Wenzangu,

Ushirikiano wetu wa karibu na bunge letu la kaunti pamoja na serikali kuu umekuwa nguzo muhimu katika kuendeleza maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha juhudi za kudumisha amani katika eneo letu.

Ushirikiano huu ndio njia pekee itakayowezesha kuleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo katika kaunti yetu.

Hakika, umoja ndio msingi wa maendeleo endelevu na ili kufanikisha haya, hatuna budi kama viongozi kuendelea kuweka mkazo kwenye masuala muhimu yanayowagusa wananchi wetu. Nawashauri viongozi wenzangu kuepuka siasa za mgawanyiko ambazo hazina manufaa kwa watu wetu.

Zaidi ya hayo, natoa wito kwa wafanyakazi wote wa kaunti kutekeleza majukumu yao, kwa bidii na uaminifu. Kila nafasi ni muhimu kwa mafanikio ya ajenda yetu ya maendeleo.

Nawahimiza kila mmoja wetu kufanya kazi kwa uadilifu na weledi, tukijitolea kwa maslahi ya kaunti yetu.

Kutotekeleza majukumu kikamilifu hakutavumiliwa, na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wale watakaopuuza au kufeli katika majukumu yao. Wananchi wanatutegemea, na matarajio yao ni kuwa tuwape huduma bora na kutimiza ahadi tulizotoa kwao.

**Mwisho,**
Tunapoadhimisha siku hii, ni muhimu kutambua kuwa mashujaa wetu si wale tu tunaojua kutoka vitabu vya historia, bali pia ni wale wanaojitolea kwa ajili ya jamii.

Mashujaa ni wale wanaotenda haki, kuchangia ustawi wa wengine, na kujenga maadili bora.

Mstakabali wa kaunti hii na nchi yetu ya Kenya umo mikononi mwa wale wanaojitolea kuleta mabadiliko katika jamii.

Hii ni fursa ya kipekee ya kujihamasisha juu ya umuhimu wa kujituma, kudumisha umoja, na kuhudumia jamii kwa dhati.

**Asanteni sana na muwe na Mashujaa yenye mafanikio!**